
UrithiWETU

12 USMJ INAVYOFANYA MAPINDUZI WILAYA KONGWE YA LIWALE

14 UMUHIMU WA MAHAKAMA KUJENGA KIZAZI CHA WATENDA HAKI

## MTO RUVUMA



Mto Ruvuma ulivyopita kati
Wilaya ya Namtumbo

# Jicho la utalii lenye hadhi ya maajabu ya dunia



Sehemu ya watalii 22 kutoka Ulaya na Marekani wakitalii katika Mto Ruvuma, kijiji cha Wenje, wilayani Tunduru

**Na Albano Midelo**

MTO Ruvuma ni miongoni mwa vivutio vitano vya utalii vinavyoubeba Mkoa wa Ruvuma. Vivutio vingine ni Ziwa Nyasa, Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, ushoroba wa Selous-Niassa, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na utalii wa kiutamaduni na kihistoria.

Mratibu wa Utalii Kanda ya Kusini, Deborah Mwakanosya anasema Mto Ruvuma umeubeba Mkoa wa Ruvuma kwa kuwa umepita katika wilaya zote tano ambazo ni Songea, Mbinga, Nyasa, Namtumbo na Tunduru.

Mwakanosya anasema Mto Ruvuma ndiyo Mto mrefu kuliko yote katika nchi za Afrika Mashariki na miongoni mwa mito maarufu barani Afrika ukiwa umeanzia kwenye misitu ya milima ya Matogoro, Manispaa ya Songea na kum waga maji yake Bahari ya Hindi.

"Mto Ruvuma umedhihirisha maajabu ya Mungu ambayo hayawezi kusimuliwa katika mikoa mingine nchini, isipokuwa Mkoa wa Ruvuma," anasema Mwakanosya na kuongeza:

"Katika milima ya Matogoro tunaku tana na chanzo cha Mto Ruvuma, ukion

Inaendelea Uk. 13

Scanned with CamScanner



boleza msibani katika jamii ya
amba.

...ula ni ngoma ambayo
... katika sherehe, sikukuu
... hususan katika kip-
...uno, mwezi wa sita na
...hadi Desemba. Kwa kuwa
...bwa ya Wandamba ni
... makanisa ya Kikristo,
...a Katoliki.

...ngoma hii huchezwa
... Krismasi, Mwaka Mpya,
... ubatizo, ndoa, sikukuu ya
... na nyinginezo.

...tahitaji ngoma hii pendwa
...aswa kujiandaa na kuan-
... kuwalipa wachezaji
...hivyo pamoja na wapigaji
...mbi, na manyanga.

...ha ngoma ya sangula
...tu kati ya 10 na zaidi.
... kuandaa chakula cha
...mbe za kienyeji kama
... mpunga, pombe ya
...rufu kama komoni,
...na nyingine.

... mwingine Wand-
...zumzaji wakubwa na
... kuzungumza kama
... kujieleza, pia asil-
...amba si washari. Hii
...ndamba hawapendi
...wakarimu.

...pindi anapoona
... sheria, na endapo
...shirikiana katika
...apo tayari kuanzisha
... kikabila, matukio
...maeneo yao yanajieleza
... kati yao na mak-
..., na hata serikali.

...wa mwanamke wa
...unza kazi mbalim-
...lea watoto na
...ake wa Kindamba
... kutwanga pepeta.
...unwa maarufu katika
... pia wanawake hao ni
... hata katika kilimo cha

... ya Wandamba ni
...enyewe wanatamka
... ambacho kinafanana
...unga kwa asilimia 69
... wa asilimia 56, hasa
...pogoro wanaoishi katika
...anga. Hii inathibitisha
... yao ni moja.

*...yumetokana na vy-
...mbali vya habari.*
*...ua bhiluka@gmail.com*

# Jicho la utalii Mkoa wa Ruvuma

Inatoka Uk. 9

chanzo hicho ni mfano wa kisima kidogo sana ambacho kimetoa mfereji mdogo lakini kazi yake huko mbele huwezi kuongelea katika hali ya kawaida na kueleweka kwa jamii.

Anasema kisima hicho kidogo chenye mfereji mdogo kwenye milima ya Matogoro kipo meta 1500 toka usawa wa bahari kimeunda mto maarufu duniani unaoitwa Ruvuma ukiwa na urefu za kilometa zaidi ya 800 na upana wa kati ya meta 300 hadi 500 kutegemea na eneo lililopo kwa sababu kuna baadhi ya maeneo mto huo una upana mkubwa zaidi.

Kwa mujibu wa mhifadhi huyo, Mto Ruvuma umebeba fukwe mbalimbali zinazovutia wageni wengi na zinapatikana kwa wingi katika hifadhi ya Taifa ya mazingira asilia ya Mwambesi iliyopo wilayani Tunduru.

Anasema katika hifadhi hiyo, Mto Ruvuma umetengeneza visiwa na fukwe nzuri za kuvutia ambazo zinamwezesha mtalii kuogelea na kuona wanyama wengi ambao wapo katika hifadhi hiyo kando kando ya Mto Ruvuma wakiwemo tembo, mamba, simba, jamii ya swala na samaki wa aina mbalimbali.

"Utakapokuwa unawashangaa wanyama katika eneo hilo na wanyama pia watakuwa wanakushangaa wewe kwa hiyo mtakuwa mnafurahi pamoja wewe na wanyama hayo ndiyo maajabu ya Mto Ruvuma", anasema Mwakanosya.

Hata hivyo Mratibu huyo wa Utalii Kanda ya Kusini anasema ili mto huo ufike katika Bahari ya Hindi na kumwaga maji yake, unaanzia wilaya ya Songea katika milima ya Matogoro, unapita katika shamba maarufu la AVIV ambalo wanaendesha kilimo cha umwagiliaji wa zao la kahawa kupitia mto Ruvuma ambapo wameajiriwa watumishi zaidi ya 3000.

Kutokea hapo mto huo umepita hadi katika eneo la Tulila, wilayani Mbinga ambako Shirika la Watawa Wakatoliki Wabenedictino wa Mtakatifu Agnes, Chipole, Jimbo Kuu la Songea wameweka mradi mkubwa wa umeme wa maji kwenye maporomoko ya Mto Ruvuma.

Akizungumza kwa niaba ya Mama Mkuu wa Shirika hilo, Sista Richards Chiwinga anasema wana mashine mbili ambazo zina uwezo wa kuzalisha megawati tano.

Hata hivyo anasema ili kufanikisha mradi huo mkubwa wa umeme Shirika lilipata ufadhili kutoka kwa raia wa Uswisi, Robert Fuchs ambaye alikopa Benki ya Dunia Dola za Marekani milioni 30 ambazo zimetumika kujenga mradi huo.

Mtawa sista Ndumbili anasema, "Hadi sasa tuna mashine mbili zenye uwezo wa kuzalisha megawati tano, lengo ni kuzalisha umeme megawati 7.5 kwa hiyo tutaongeza mashine moja yenye uwezo wa kuzalisha megawati 2.5".

Analitaja bwawa la Tulila kuwa lina ukubwa wa meta za ujazo milioni 1.14, likiwa na urefu wa meta 750 kutoka usawa wa bahari na usawa wa maji (level) ni meta 748 na kwamba maji yakizidi kiwango hicho yanamwagika.

Kulingana na Sista Ndumbili, shirika katika eneo hilo la Tulila linamiliki eneo lenye ukubwa wa ekari 1,000 ambapo wanatarajia pia kuweka maeneo mazuri kwa ajili ya fukwe za kupiga picha, kufanya pikiniki na kuogelea, lengo likiwa ni kufungua milango ya utalii kwa wageni wa ndani na nje ya nchi katika eneo hilo.

Tulila katika maporomoko ya Mto Ruvuma ni eneo lenye mandhari nzuri ya kuvutia unaweza kufanya utalii wa kupiga picha, kuogelea, kuendesha mtumbwi, pia kuna fukwe nzuri kutoka katika Mto Ruvuma ambao ni miongoni mwa mito maarufu barani Afrika ambao unamwaga maji yake Bahari ya Hindi.

Mto Ruvuma katika Wilaya ya Nyasa umepita kwenye Pori la Akiba la Liparamba ambako katika eneo la Nakatuta kuna maporomoko mazuri ya maji ya Mto Ruvuma ambayo yanavutia wageni wengi.

Katika eneo hilo pia mtalii anaweza kufanya utalii wa kuvua samaki na kupanda kwenye tabaka la jiwe kando kando ya Mto Ruvuma.

Kulingana na mtalaam huyo wa uhifadhi safari ya Mto Ruvuma kutoka Liparamba imeendelea hadi eneo la Mkenda mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ambako kumejengwa daraja kubwa lenye urefu wa meta 98 linalogawa Tanzania na Msumbuji kupitia Mto Ruvuma.

Mwakanosya anabainisha zaidi kuwa Mto Ruvuma umeendelea hadi katika Wilaya ya Namtumbo katika jumuiya za uhifadhi wanyamapori vijijini ambazo ni Kimbanda, Kisungule na Chingoli na kwamba Mto Ruvuma unaendelea hadi katika Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Mwambesi uliopo wilayani Tunduru.

"Mto Ruvuma katika Hifadhi ya Mwambesi kuna vivutio vya aina zote ikiwemo michezo ya kuendesha mitumbwi ambayo kwa mara ya kwanza nchini ilizinduliwa mwaka 2019 katika eneo la Wenje katika mto huo na watalii 22 ambao walitoka nchi 16 duniani walishiriki", anasisitiza Mwakanosya.

Anasema mto huo ukishapita katika wilaya zote za mkoa wa Ruvuma unaendelea na safari yake hadi katika Daraja la Umoja wilayani Nanyumbu, mkoani Mtwara na kuendelea hadi mkoani Mtwara.

Mto Ruvuma unamwaga maji yake katika Bahari ya Hindi kwenye eneo la kati ya Mtwara nchini Tanzania na Rasi ya Delgado nchini Msumbiji. Hata hivyo historia inaonesha kuwa Mto Ruvuma pia ulitumika katika biashara ya watumwa ambapo watu waliokuwa wanafanya biashara ya utumwa walianzia katika nchi ya Msumbiji kupitia Mto Ruvuma njia ya Daraja la Mkenda ambapo walisafiri hadi katika soko la watumwa Mikindani na Kilwa na watumwa kupakiwa kwenye meli hadi nchi nyingine.


Wadau wa utalii mkoani Ruvuma wamewapongeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wilayani Songea kwa kuendelea kuhifadhi na kutunza chanzo cha Mto Ruvuma ambacho leo kimekuwa kivutio adimu cha utalii duniani.

Denisi Moyo ni mmoja wa wadau wa utalii mkoani Ruvuma, anasema hata kama haijatangazwa rasmi, Mto Ruvuma ni moja ya maajabu ya dunia.

Moyo anasema sababu ya hoja yake hiyo ni kutokana na namna mt huo ulivyoanza kama kisima kidogo sana lakini umetanuka na kuwa na urefu wa zaidi ya kilometa 800 na upana wa zaidi ya meta 400 ukiwa na vivutio vingi.


"Kumbe Mto Ruvuma ni moja ya maajabu duniani, natoa rai kwa Wizara ya Maliasili na Utalii ingesaidia kuutangaza rasmi mto huu ili kuongeza ajira na mapato kwa mkoa na taifa kupitia sekta ya utalii", anasema Moyo.


*Mawasiliano: albano.midelo@gmail.com*



**Hiki ndiyo chanzo cha Mto Ruvuma kilichopo milima ya Matogoro, Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma.**

**Maporomoko ya Mto Ruvuma katika eneo la Tulila wilayani Mbinga ambako kuna mradi wa umeme wa kutumia maji. Watu mbalimbali hufanya utalii**





**Maporomoko ya Nakatuta katika Mto Ruvuma ndani ya po... paramba wilayani Nyasa ni moja ya kivutio cha utalii.**